# TUNAAJIRI!

## MAAFISA WA MAUZO (NAFASI 4)

USINDO Ventures Limited inatafuta Maafisa wa Mauzo wenye bidii, uaminifu na uwezo wa kujenga mahusiano ya muda mrefu na wateja ili kusaidia upanuzi wa biashara ya USINDO Fresh Fish jijini Dar es Salaam.

Lengo letu ni kuongeza mauzo kutoka kilo 1,500 hadi kilo 6,000 kwa wiki kupitia upatikanaji wa wateja wapya wa jumla.

### Taarifa za Kazi

| | |
|---|---|
| Mkataba | Miezi 3 (unaoweza kuongezwa kulingana na utendaji) |
| Kituo cha Kazi | Makuburi, Ubungo, Dar es Salaam |
| Idadi ya Nafasi | 3 |

### Majukumu Makuu

- Kutafuta na kusajili wateja wapya wa samaki wa jumla.
- Kutembelea maduka ya samaki, migahawa, hoteli, taasisi na wafanyabiashara wakubwa.
- Kutangaza bidhaa na huduma za USINDO Fresh Fish.
- Kukusanya taarifa za soko na bei za washindani.
- Kuandaa ripoti za kila siku na kila wiki.

### Malengo ya Kazi (KPIs)

| **Kigezo** | **Lengo** |
|---|---|
| Ziara za wateja watarajiwa | Angalau 10 kwa siku |
| Wateja wapya hai (Active Customers) | Hadi 10 kwa wiki |
| Kiwango cha chini cha ununuzi kwa kila mteja | Kilo 50 kwa wiki |
| Mauzo mapya | Angalau kilo 400 kwa wiki |
| Ripoti za mauzo | Kila siku na kila wiki |

Mteja hai (Active Customer) ni mteja anayenunua samaki kutoka USINDO Fresh Fish kila wiki kwa kiwango kisichopungua kilo 50.

### Sifa za Mwombaji

- Form four, form six, diploma au Cheti katika Biashara, Masoko au fani inayofanana.
- Uzoefu wa mauzo ni faida ya ziada.
- Uwezo mzuri wa mawasiliano na ushawishi.
- Mwaminifu, mwenye nidhamu na anayependa kufanya kazi kwa malengo.
- Kufahamu maeneo ya Dar es Salaam ni faida.
- Kumiliki simu ya Android.
- Kujua kuendesha pikipiki ni faida.

### Maslahi

- Mshahara: TSh 200,000 kwa mwezi. Mshahara utaongezeka baada ya miezi miwili.
- Posho ya usafiri na mawasiliano: TSh 25,000 kwa siku za kazi.
- Mafunzo ya awali kuhusu bidhaa na mbinu za mauzo.

- Fursa ya kuendelea na ajira kulingana na utendaji.

## Bonasi ya Utendaji

Afisa wa Mauzo atalipwa bonasi ya TSh 100,000 kwa mwezi endapo atatimiza masharti yafuatayo:

- Atapata wateja hai wanaonunua kwa pamoja angalau kilo 200 kwa wiki zaidi ya lengo la awali la kilo 400 kwa wiki.

## Jinsi ya Kutuma Maombi

Tuma CV na barua ya maombi kupitia:

Barua pepe: usindoventuresltd@gmail.com

Tuma maombi wa whatsapp number: +255752040521

Kichwa cha barua pepe: Maombi ya Afisa wa Mauzo

## Mwisho wa Kutuma Maombi

10 Agosti 2026